

TANGAZO LA SERIKALI Na. 325 la tarehe 28/4/2023

SHERIA YA MIPANGOMIJI
(SURA YA 355)

AMRI

(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 8(1))

AMRI YA KUPANGA ENEO LA NSHINDE YA MWAKA 2023

Jina

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Kupanga Eneo la Nshinde ya Mwaka 2023.

Utangazaji wa eneo la upangaji Sura ya 355

2. Eneo lililoainishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa eneo la upangaji kwa madhumuni ya Sheria ya Mipangomiji.

Mpango wa jumla na kina wa eneo

3. Mipango ya jumla na kina ya eneo lililoainishwa katika Jedwali inaandaliwa na kuhifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Mipangomiji na Mkurugenzi wa Mji wa Geita.

—
JEDWALI
—

(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)

Eneo la upangaji lipo ndani ya mipaka ifuatavyo-

“Unaanzia kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba A yenyemajira-nukta 420898MS, 9679277KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini katika uelekeo wa 57⁰ kwa umbali wa kilometa 1.48 kupitia barabara ya Mwatulole - Magogo hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba B yenye majira - nukta 419510MS, 9679812KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini katika uelekeo wa 105⁰ kwa umbali wa kilometa 1.62 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba C yenye majira - nukta 418556MS, 9678500KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini – Mashariki katika uelekeo wa 87⁰ kwa umbali wa kilometa 0.81 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba D yenye majira-nukta 419238MS, 9678053KZ’ hadi ulipoanzia””

Dodoma,
17 Machi, 2023

ANGELINE S. MABULA,
*Waziri wa Ardhi, Nyumba na
Maendeleo ya Makazi*